# MSUMENO WA VISU VINGI KWA AJILI YA KUPASUA (KUVUNJAVUNJA) MAGOGO

PANDA MITI KIBIASHARA
PRIVATE FORESTRY PROGRAMME

## Taarifa za ujumla

- Msumeno wa kupasua magogo umebuniwa kwa ajili ya uharaka na ubora wa kuchana mbao na hasa kwa magogo ya kipenyo kidogo (10-25cm)
- Mashine ya kuchana mbao kwa ukubwa tofauti inaweza kutumika kuchana vipande vya mbao vilivyochanwa na mashine ya kupasua magogo.
- Mashine inaweza kutumika kwa aina zote za mbao ngumu na laini.
- Matumizi ya misumeno mduara mingi kwa wakati mmoja inakuhakikishia kasi ya uhakika ya upasuaji mbao.
- Mashine zote zinatumia mfumo unaojiendesha kuweka mbao katikati ili kupungusha upotevu wa mbao unaofikia hadi asilimia 45.
- Mashine zote zinanafasi iliyopimwa, inayowezesha ubadilishwaji wa visu kulingana na ukubwa unaohitajika.
- Mfumo wa uingizaji gogo unaweza kutanuka kutokana na aina au ukubwa wa gogo kuingia kwa spidi anayoitaka mwendeshaji.



## Vipimo na gaharama za matengenezo

- Msumeno unauwezo wa juu wa kuchana mita za ujazo 15 kwa awamu moja (ikiwa na wendeshaji 4 kwa saa nane za kazi)
- Ukubwa wa misumeno yote miwili ni milimita 2900x1400x1600 (urefu—upana—kimo) ikiwa na sehemu ya kupokelea magogo yenye ukubwa wa mita 5.
- Uzito wa msumeno ni kilo 800 na msumeno unaorudia kuchana ni
- Mashine inaweza kukata magogo yaliyo kati ya sentimeta 10—15.
- Kipenyo cha msumeno ni milimita 355 ukiwa na tundu katikati lenye ukubwa wa milimita 50 na meno yenye milimita 18 wakati ukubwa wa msumeno unaorudia kuchana mbao ni milimita 250 x 50 na meno ya milimita 24
- Mashine inayoanza kupasua gogo inauwezo wa kuzungusha msumeno kwa kasi ya mizunguko 3,000 kwa dakika, wakati mashine inayorudia kupasua mbao inauwezo wa kuzungusha kisu mara, 4,500 kwa dakika.
- Mahitaji ya umeme kwa mashine inayoanza kupasua gogo ni 62kWh na 57kWh kwa mashine inayorudia kuchana mbao.
- Kabla ya kuanza kazi, kiungo cha mpira wa maji ya kupooza kihakikiwe na kukaguliwa kila wakati.
- MIsumeno ikazwe, inolewe na kurekebishwa kila baada ya saa 1-2.
- Mashine ikaguliwe vilainishi kila siku kabla ya kuanza kwa shughuli za uzalishaji.
- Unga wa mbao unaobakia kwenye mashine na boksi la umeme utolewe kila siku.
- Beringi za mashine zibadilishwe walau mara moja kwa mwaka, au mapema zinapoharibika.









## Taarifa za manunuzi

- Mashine hizi zinanunuliwa Uchina, pia zinapatikana nchini Ufini
- Zifuatazo ni gaharama za kununua:
  - Bei ya kununua (inajumuisha gharama za usafishaji na bima) kwa msumeno wa kupasua magogo ni Yuro: 17,000 na unaorudia kuchana mbai ni Yuro 16,000.
  - Kodi ya kuingiza ncini ni asilimia 27
  - Kodi ya ongezeko la thamani kwa kununua na kwa kodi ya kuingizwa nchini ni asilimia 18
  - Gharama za utoaji mzigo bandarini ni Yuro 800
  - Gharama za ndani za usafirishaji ni Yuro 1,400 kwa kila mashine.
- Mambo ya kuzingatia kabla ya kununua mashine:
  - Uwezo
  - Upatikanaji wa vipuli
  - Upatikanaji wa waendeshaji wenye ujuzi
  - Hati ya kutengeneza/kubadilisha (Warranty)
  - Utaratibu wa matengenezo ya mashine

## Taarifa za gharama na faida

| Maelezo | Msumeno wa kupasua magogo | Msumeno wa kuchana mbao |
|---|---|---|
| Uendelevu | Mbao na samani za kati na utengenezaji wa viungo | |
| Gharama za uwekezaji | Yuro 27,000 | Yuro 25,000 |
| Idadi ya waendeshaji | 2 | 2 |
| Umeme | 62 kWh (makadirio 40 kWh) | 57 kWh (makadirio 30 kWh) |
| Gharama za umeme (kwa mwezi, kwa kuzingatia awamu moja ya masaa 8, katika siku 5 za kazi | Tsh milioni 2,2 (kulingana na makadirio ya kati) | Tsh milioni 1,7 (kulingana na makadirio ya kati) |
| Matengenezo | Kila siku (kabla ya kuwashwa): kagua mabomba ya maji, vilainishi na beringi, safisha boksi la umeme, kagua meno ya msumeno na noa visu/misumeno (zana hitajika: mashine ya kunoa misumeno, vilainishi)<br>Mwezi: rekebisha silinda ya mgandamizo wa hewa (zana hitajika: kifaa cha kusomea mita)<br>Mwaka: badili beringi za mashine (zana hitajika:beringi, misumeno, vilainishi) | |
| Gharama za matengenezo kwa mwezi (kwa mfumo mzima) | Malipo ya wafanya kazi, TSH 36,000 Vipuli TSH 40,000, Gharama za kunoa msumeno TSH200,000 | |
| Kiwango cha juu cha uzalishaji kwa mwaka | Mita za ujazo 3,600 | |

## Huduma za kituo zinazohusiana na kituo cha mafunzo

- Kupima sampuli za mbao za mteja.
- Huduma za maelezo kwa wadau na wateja wenye lengo la kununua.
- Huduma za ushauri wadau na wateja wenye lengo la kununua.
- Mafunzo kwa wamiliki wa viwanda, mameneja na waendeshaji juu ya matumizi ya
- Mafunzo juu ya upasuaji sahihi wa mbao na namna ya kupunguza uharibifu wa mbao. (recovery rete).

## Mawasiliano na namna ya kufika kituoni

Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazeo ya Misitu (KMVMM)

Kinyanambo

Mafinga

Mr. Edigary, Mwaifweya Meneja wa Kituo.

Barua pepe: edigary.mwaifweya@privateforestry.or.tz

Tel: +255 744 874 521

Maelezo kwa watumiaji magari: Njia panda ya kituo cha Mafuta cha CF, barabara iendayo Madibira, endesha umbaki wa kilomita moja. Utaona kibao cha kituo upande wa kushoto mwa barabara, mkabala na kiwanda cha mkaa.

## Kuhusu Programu ya Panda Miti Kibiashara PFP)

Pandamiti Kibiashara husaidia umiliki binafsi wa mashamba ya miti hasa katika uanzishwaji na utunzaji wa mashamba ya miti kwa wakulima wadogo, kadhalika viwanda vya mazao ya misitu pamoja na ukuaji wa soko la mazao ya mbao yaliyokomaa ambayo yatanufaisha wadau wote. Programu inatekeleza katika Mikoa minne: Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma.

Mradi unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finaland na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania.

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

FORMIN.FINLAND.FI
MINISTRY FOR FOREIGN AFFAIRS OF FINLAND

© Private Forestry Programme 2018